

TAARIFA YA UKAGUZI WA MIRADI

Tar. 25 Feb. 2021

1) SHULE YA SEKONDARI MWANDEGE

Ujenzi wa madarasa 05 na matundu 12 ya vyoo.

- Hali ya Mradi kwa sasa
 - a) Ujenzi wa madarasa 05 unaendelea, ambapo;
 - Madarasa 02 yamepauliwa na kuwekwa jamvi. Kazi zilizobaki ni kupiga bati, kuweka floor na ubao wa kuandikia. Kazi ya kupiga bati inatarajiwa kuanza leo tar. 25/02/2021. Madarasa haya yanatarajiwa kukamilika tar. 27/02/2021.
 - Madarasa 03 yapo hatua ya kufunga renta. Ujenzi wa madarasa haya unatarajiwa kukamilika tar. 03/03/2021 kutokana na changamoto ya upatikanaji wa bati zinazopendekezwa kiwandani.
 - b) Ujenzi wa matundu 12 ya vyoo unaendelea, ambapo;
 - Ujenzi wa matundu 6 kwa ajili ya vyoo vya wavulana upo hatua ya kufunika shimo. Kazi zilizobaki ni kufunika shimo kwa zege Pamoja na kujenga jengo la choo (toilet block).
 - Ujenzi wa matundu 6 kwa ajili ya vyoo vya wasichana upo hatua ya kupanga tofali kwenye shimo. Kazi zilizobaki ni kufunika shimo kwa zege Pamoja na kujenga jengo la choo (toilet block).
- Matumizi ya Fedha za Mradi

Jumla ya Tshs. 29,929,613.00 zimetumika kati ya Tshs. 64,000,000.00 zilizopokelewa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 05. Aidha, Tshs. 12,000,000.00 za ujenzi wa choo bado hazijatumika kutokana na makubaliano ya kufanyika malipo baada ya ujenzi kukamilika.
- Upatikanaji wa Vifaa vya Ujenzi katika eneo la ujenzi

Vifaa vyote vya ujenzi kwa ajili ya madarasa yote 05 ikiwemo nondo, kenchi, cement, na matofali vipo katika eneo la ujenzi. Aidha, bati zilizopo ni kwa ajili ya madarasa 02 na choo tu. Bati za madarasa 03 zinatarajiwa kufika kutoka kiwandani kuanzia tar. 01/03/2021.
- Changamoto za Mradi

Zipo sababu mbalimbali zilizochelewesha ukamilishaji wa miradi hii kwa wakati, ikiwemo ucheleweshwaji wa BOQ kwa ajili ya ujenzi wa choo Pamoja na kukosekana kwa material ya kutengenezea bati zilizopendekezwa kiwandani.

➤ Muonekano wa Miradi yote katika Picha.



Maandalizi ya kupiga bati katika madarasa 02 katika shule ya sekondari Mwandegé.

Muonekano wa madarasa hayo 02 kwa ndani.



Hali ya ujenzi wa madarasa 03 ukiwa hatua ya kufunga rinta.

Muonekano wa madarasa 03 kwa ndani.



Ujenzi wa matundu 06 ya vyoo vya wavulana.

Ujenzi wa matundu 06 ya vyoo vya wasichana.

2) SHULE YA SEKONDARI TAMBANI

Ujenzi wa madarasa 06 na matundu 07 ya vyoo.

- Hali ya Mradi kwa sasa
 - a) Ujenzi wa madarasa 06 unaendelea, ambapo;
 - Madarasa 03 yamepigwa bati na kuwekwa jamvi. Kazi zilizobaki ni kuweka floor na ubao wa kuandikia. Kazi za kuweka floor na ubao zinatarajiwa kuanza tar. 26/02/2021. Madarasa haya yanatarajiwa kukamilika tar. 27/02/2021.
 - Madarasa 02 yamepauliwa. Kazi zilizobaki kwenye madarasa haya 02 ni kupiga bati, kujaza kifusi ndani na nje, kumwaga jamvi, kuweka floor na ubao. Kazi hizi zinatarajiwa kukamilika tar. 06/03/2021.
 - Darasa 01 lipo hatua ya kufunga rinta. Kazi zilizobaki kwenye darasa hili 01 ni kujenga gebo, kupiga bati, kujaza kifusi ndani na nje, kumwaga jamvi, kuweka floor na ubao. Kazi hizi zinatarajiwa kukamilika tar. 06/03/2021.
 - Ujenzi wa matundu 07 ya vyoo unaendelea, ambapo upo hatua ya kufunika shimo pamoja na kujenga jengo la choo (toilet block). Kazi hii inatarajiwa kukamilika tar. 06/03/2021.
- Matumizi ya Fedha za Mradi

Jumla ya Tshs. 28,300,000.00 zimetumika kati ya Tshs. 64,000,000.00 zilizopokelewa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 06. Aidha, Tshs. 7,000,000.00 za ujenzi wa choo bado hazijatumika kutokana na makubaliano ya kufanyika malipo baada ya ujenzi kukamilika.
- Upatikanaji wa Vifaa vya Ujenzi katika eneo la ujenzi

Vifaa vyote vya ujenzi kwa ajili ya madarasa yote 06 na matundu 07 ya vyoo ikiwemo nondo, kenchi, cement, bati na matofali vipo katika eneo la ujenzi.
- Changamoto za Mradi

Hakuna.

➤ Muonekano wa Miradi yote katika Picha.



Muonekano wa madarasa 03 katika shule ya sekondari Tambani.



Muonekano wa ndani wa madarasa hayo 03.



Ujenzi wa madarasa 02 ukiendelea.



Ujenzi wa darasa 01 ukiendelea.



Ujenzi wa matundu 07 ya vyoo ukiendelea.